Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 22, AGOSTI 2024






# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**WAHARIRI WASAIDIZI**
Emmanuel Malegi
Atley Kuni

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge
Aisha Swahibu
Atley Kuni

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

Bilioni 5 kujenga hospitali ya rufaa mkoa wa Morogoro ….Uk 2





Hakikisheni huduma za matibabu ya kibingwa Zinawafikia wananchi wa hali ya chini…. Uk 3

Shirikianeni katika utoaji wa huduma bora za afya ili Kukabiliana na magonjwa ya mlipuko….. Uk 4





Toeni elimu zaidi kwa wananchi juu ya ugonjwa wa mpox; waziri mhagama…. Uk 5

Serikali kuendelea kushirikiana na who kuboresha Sekta ya afya ….. Uk 6





Tanzania ni salama, hakuna ugonjwa wa mpox…. Uk 6

Hospitali zote nchini zaagizwa kuhudumia mgonjwa Kwa masaa yasiyozidi matatua…… Uk 7





# BILIONI 5 KUJENGA HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA MOROGORO

**Na. Hassan Kimweri**
**MOROGORO**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameagiza kujengwa kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro kwa kuanza ujenzi wa jengo la Afya ya uzazi mama na mtoto ili kurahisha upatikanaji wa huduma hizo.

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema hayo Agosti 6, 2024 akiongea na wananchi wa mkoa wa Morogoro wakati akihitimisha ziara yake mkoani humo baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kiwanda cha 'Serengeti Cigarette Company' (SCC) pamoja na kuzindua jengo le Maabara jumuishi Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

"Nataka nikubaliane nanyi kwamba sasa, Hospitali tuliyonayo haikidhi vigezo vya kuwa Hospitali ya Rufaa ya mkoa kwa ulimwengu wa leo, hivyo basi nimempa maelekezo Waziri wa Afya apate Bilioni 5 za kuanzia ujenzi wa Hospitali ya Rufaa." Amesema Rais Samia.

Amesema, Hospitali hiyo itaanza kujengwa majengo makubwa ya mama na mtoto zikiwa na vifaa vyote vya kutolea huduma hizo ikiwemo vyumba vya upasuaji pamoja na wodi ya uangalizi maalum (ICU), kisha kufuatia wodi nyingine hadi kukamilika kwa Hospitali hiyo.

Aidha, Rais Samia amesema Serikali kupitia Wizara ya Afya imejenga vituo vya Afya 136 ili kurahisha huduma za Afya ikiwemo huduma za mama na mtoto katika mkoa wa Morogoro.

"Vituo hivi vinasaidia sana lakini lile ombi la Mbunge wa Jimbo la Morogoro mjini Mhe. Abdul-Aziz Abood la kuwa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya kisasa tunakwenda kuliteleza." Amesema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan

# HAKIKISHENI HUDUMA ZA MATIBABU YA KIBINGWA ZINAWAFIKIA WANANCHI WA HALI YA CHINI

**Na. Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amewataka wafanyakazi wa wizara hiyo kuhakikisha huduma za kibingwa za matibabu ya magonjwa mbalimbali zinawafikia wananchi wa hali ya chini bila ya kuwa na vikwazo vyovyote.

Waziri Mhagama ametoa kauli hiyo Agost 15, 2024 jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na Manejimenti na watumishi wa wizara hiyo katika ofisi ndogo za wizara ya Afya mara baada ya kuapishwa ikulu mchana wa leo.

Waziri Mhagama amesema Serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa vifaa tiba vya kisasa, kujenga majengo ya kisasa, kusomesha wataalamu na kuboresha maslahi ya wafanyakazi jukumu lililobaki kwao ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za matibabu.

"Kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali yetu asilimia 95 ya huduma za matibabu ya kibingwa zinapatikana hapa nchini ni jukumu lenu kuhakikisha uwekezaji huu uliofanywa na Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan unawafikia wananchi wengi zaidi waliopo ndani na nje ya nchi yetu" Amesema Waziri Mhagama.
Pia amesisitiza watoa huduma za afya kuendeleza matumizi bora ya lugha za staha na kuimarisha mawasiliano na wagonjwa katika maeneo yao ya kutolea huduma.

"Kuna wakati mgonjwa anahitaji kupata maneno mazuri ya faraja na akipata mane no hayo kwa asilimia kubwa anakuwa na matumaini ya kupona ugonjwa wake, tunahitaji kuwasaidia watanzania kwani sisi tumebeba usalama wa afya za watanzani hivyo basi tutimize wajibu wetu wa kazi kwa kufuata sera na miongozo iliyopo", Amesema Waziri Mhagama.

Akizungumzia kuhusu tiba utalii Mhe. Mhagama alisema miaka michache iliyopita hakukuwa na uwekezaji wa kutosha katika sekta ya afya kutokana na uwekezaji uliofanyika wananchi kutoka nchi za jirani wanakuja kutibiwa hapa nchini.
"Mimi na viongozi wenzangu tutatoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha wizara yetu inakwenda mbele zaidi na kutoa huduma bora kwa watanzania na wasio watanzania ambao wanakuja katika nchi yetu kupata huduma za matibabu", Amesema Waziri Mhagama.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya Mhe. Godwin Mollel alimpongeza Waziri Mhagama kwa kuteuliwa kuwa waziri wa wizara hiyo na kusema kuwa uzoefu aliokuwa nao utasaidia kuifikisha wizara hiyo mbali Zaidi huku Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. John Jingu akisema kazi kubwa ya wizara ya Afya ni kuzuia magonjwa, kutibu na kupambana na magonjwa yanayoibuka pamoja na kutekeleza majukumu mengine yaliyopo ya kuhakikisha usalama wa afya unakuwepo nchini.





# SHIRIKIANENI KATIKA UTOAJI WA HUDUMA BORA ZA AFYA ILI KUKABILIANA NA MAGONJWA YA MLIPUKO

**Na Shabai Juma**
**SONGWE**

Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, amewataka watumishi wa afya kushirikiana kwa karibu katika utoaji wa huduma za afya ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Dkt. Mollel ametoa wito huo Agosti 22, 2024 alipokuwa akitembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe leo, ambapo amefanya ziara ya kukagua hali ya utoaji wa huduma na utayari wa hospitali hiyo katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Dkt. Mollel amesisitiza kuwa ushirikiano miongoni mwa watumishi ni msingi wa utoaji wa huduma bora kwa wananchi huku akisisitiza kuwa, kila mtumishi anapaswa kushiriki kikamilifu katika majukumu yake na kufanya kazi kwa kushirikiana na wengine ili kuongeza ufanisi katika huduma zinazotolewa.

"Shirikianeni katika kutoa huduma za afya, kufanya kwenu vizuri kunaletwa na ushirikiano mlionao, mkiwa kitu kimoja ni rahisi kutoa huduma kwa pamoja," Amesema Dkt. Mollel.

Aidha, Dkt. Mollel ameeleza kuwa Serikali imewekeza katika miundombinu na vifaa vya kutosha kwa lengo la kuboresha huduma za afya, na hivyo akawataka watumishi kufanya kazi kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa.

Pia, Dkt. Mollel ameipongeza Menejimenti ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe kwa usimamizi mzuri wa hospitali hiyo na akatoa rai kwao kuendelea kuchapa kazi kwa bidii.

Ziara ya Dkt. Mollel katika hospitali hiyo imekuja wakati ambapo Serikali inaendelea na juhudi zake za kukabiliana na magonjwa ya mlipuko pamoja na kuboresha huduma za afya nchini, hususan katika maeneo ya pembezoni

# TOENI ELIMU ZAIDI KWA WANANCHI JUU YA UGONJWA WA MPOX; WAZIRI MHAGAMA

**Na Majid Abdulkarim**
**ARUSHA**

Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama amewataka wataalamu wa Afya nchini kuongeza kasi ya kutoa elimu ya ugonjwa wa Mpox ili wananchi wawe na uelewa mpana dhidi ya ugonjwa huo.

Waziri Mhagama ametoa agizo hilo Agosti 21, 2024 wakati wa ziara kwenye Kituo cha Forodha cha Mpaka wa Namanga Halmashauri ya Wilaya ya Longido mkoani Arusha alipofika kuona utayari wa kukabiliana na ugonjwa wa Mpox.

“Nimezungumza na mmoja wa wasafiri lakini hajui dalili za ugonjwa wa Mpox hivyo ipo haja ya kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa wananchi ili kuwa na uelewa juu ya ugonjwa huo”, ameeleza Mhe. Mhagama na kuongeza

"Kuwe na mabango na vipeperushi vinavyotoa elimu juu ya ugonjwa kuelezea Dalili, unaambukizwaje na namna ya kujikinga ili kila msafiri anayeingia na kutoka nchini awe na uelewa mpana" amesisitiza Waziri Mhagama.


Mhe. Mhagama amesema kwa sasa mpaka Tanzania ni Salama na hakuna mgonjwa yeyote aliyebainika kuwa na ugonjwa huo hivyo wananchi waendelee kuchukua tahadhari juu ya ugonjwa wa Mpox.

“Natoa wito kwa wananchi kila mmoja awe mlinzi kwa mwenzake pale atakapo ona dalili za ugonjwa huo kwa mtu basi atoe taarfa kwa wataalamu wa afya, Kituo cha kutolea huduma za afya kilichopo karibu yake au kuwasiliana na Wizara ya Afya kwa Namba ya 199 ili kuhakikisha nchi inakuwa salama”, ametoa wito.

Akihitisha ziara yake Waziri Mhagama amewahakikishia watanzania kuwa Wizara yake imejipanga kikamilifu kwa kuimarisha Huduma za uchunguzi na maabara maeneo ya mipakani ili kuhakikisha ugonjwa huo hauingii nchini



# SERIKALI KUENDELEA KUSHIRIKIANA NA WHO KUBORESHA SEKTA YA AFYA.




**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DAR ES SALAAM**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu Amesema serikali kupitia Wizara ya Afya itaendelea kushirikiana na Wadau wa maendeleo katika sekta ya afya nchini akiwemo Shirika la Afya Duniani WHO ili kuhakikisha watu wote wanapata huduma bora za afya.

Dkt. Jingu ameyasema hayo Agosti 2, 2024 Jijini Dar es salam Wakati makabidhiano ya vitanda 65 vya wagonjwa wa kipindupindu kutoka WHO kwenda Tanzania ikiwa ni sehemu ya lengo la kuimarisha Mapambano dhidi ya Magonjwa ya Mlipuko Nchini kwa sasa na yajayo ikiwemo kipindupindu na dharura kama hizo nchini Tanzania.

Dkt. Jingu amesema mashirikiano baina ya Wizara ya Afya na WHO yanalenga kuimarisha mashirikiano katika kuwajengea uwezo watoa huduma za Afya na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini ili kufikia lengo la utoaji wa huduma bora za Afya Nchini.

“WHO mmekuwa wadau Muhimu Katika eneo hili na kuhakikisha watu wote wanapata huduma nzuri za Afya, Moja ya mambo ni kuhakikisha tunawajengea uwezo wataalam wetu kwa kuwapatia mafunzo stahiki, nakuhakikisha tuna miundombinu mizuri pamoja na viafaa vyote na mahitaji yatayosaidia huduma husika ziweze kutolewa, na leo hapa tunapokea baadhi ya vifaa hivyo ambavyo vitawezesha watoa huduma wetu kutimiza majukumu yao” amesema Dkt. Jingu.

Ameongeza kuwa mashirikiano hayo pia yanakuwa chachu ya utayari wa muda wote wa pamoja wa kupambana na magonjwa yanayolipuka nchini ambapo WHO wamekuwa wadau wakubwa na Serikali inajivunia Kushirikiana nao.

Aidha Dkt. Jingu amewashukuru WHO kwa kuwa na utayari wa muda wote na kuendelea kushirikiana na wizara ya afya na Serikali ya Tanzania Kwa Ujumla na kuwasihi kuendelea kufanya hivyo ili kuchochea matokeo chanya katika sekta ya afya nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa WHO Nchini (Tanzania) Dkt. Charles Sagoye – Moses amesisitiza kuwa wito wao ni kuimarisha na kuendelea na utekelezaji wa mbinu mbalimbali za kisekta za kuzuia na kudhibiti magonjwa ya mlipuko nchini ikiwemo Kukomesha kipindupindu kwa kushirikiana na Serikali na jamii nzima.



# TANZANIA NI SALAMA, HAKUNA UGONJWA WA MPOX

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**KIGOMA**

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu ametoa taarifa ya mwenendo wa ugonjwa wa MPOX na kuwaondoa hofu watanzania kuhusu uwepo wa ugonjwa huo hapa nchini na kuwasisitiza watanzania Kuendelee kuchukua tahadhari.

Prof. Nagu ameyasema hayo Agosti 17, 2024 kwenye taarifa aliyoitoa kwa wananchi na kuelezea jitihada mbalimbali zinazofanywa na Wizara ya Afya kufatilia na kuhakikisha ugonjwa huu hauingi nchini na kupata taarifa zote zinazohusu mwenendo wa ugonjwa wa MPOX hapa nchi. pamoja na

"Mpaka sasa, hakuna mgonjwa yeyote aliyethibitika kuwa na maambukizi ya Mpox na nchi yetu ni salama, hata hivyo niwasisitize wananchi kuchukua tahadhari kwani tayari shirika la Afya Duniani limetangaza kuwa hili ni janga la dharura." Amesema Prof. Nagu

Prof. Nagu amesema kuwa kwa sasa nguvu kubwa inaelekezwa kwenye elimu ya kutambua dalili mbalimbali za ugonjwa wa MPOX na itatolewa kwa njia mbalimbali ili iweze kuwafikia wananchi kwa haraka.

"Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuzuia kuingia nchini ugonjwa wa MPOX na kuimarisha utayari wa kukabiliana nao, hii ni pamoja na kuandaa na kusambaza vipeperushi vya elimu ya jamii kuhusu dalili na njia za kujikinga na ugonjwa wa MPOX, vilevile, wizara imeimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa ugonjwa huu katika ngazi zote." Amesema Dkt. Nagu

Aidha Prof. Nagu ameelezea tahadhari mbalimbali za kuchukua ili kujikinga na ugonjwa wa MPOX.

"Tunahitaji kuendelea kuchukua tahadhari kujikinga na ugonjwa huu kwa kutekeleza yafuatayo endapo unamuona mtu anadalili za Mpox, Toa taarifa kwa kupiga simu namba 199 bila malipo, epuka kugusa majimaji ya mwili au ngozi ya mtu mwenye dalili za ugonjwa wa Mpox, epuka kugusana, kusalimiana kwa kupeana mikono, kukumbatiana na kumbusu mtu mwenye dalili za Mpox, nawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono mara kwa mara, epuka kula au kugusa mizoga au wanyama mfano nyani au swala wa msituni, Vaa barakoa iwapo itabidi kukaa na kuongea kwa karibu na mtu mwenye dalili za Mpox, Kuwahi katika vituo vya huduma za afya unapoona dalili za ugonjwa wa Mpox." Amesema Prof. Nagu

# HOSPITALI ZOTE NCHINI ZAAGIZWA KUHUDUMIA MGONJWA KWA MASAA YASIYOZIDI MATATU

**Na Domina Jacob**
**DODOMA**

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amezitaka Hospitali zote na vituo vya Afya nchini kuhudumia wagonjwa wa nje wanaofika kupata huduma kwa masaa yasiyozidi matatu.

Waziri Jenista amesema hayo Agosti 20, 2024 wakati alipotembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma (General) ili kuona hali ya utoaji wa huduma sambamba na kuongea na watumishi waliopo Hospitalini hapo.

Amezitaka Hospitali zote nchini na kuziagiza kuzingatia mzunguko wa utoaji wa huduma kwa wagonjwa na kuhakikisha mzunguko huo unatumia masaa ya kitaalamu ambayo hayazidi masaa matatu kwa kila mgonjwa na kupunguza muda wa wagonjwa kukaa hospitali kusubiri huduma.

"Mgonjwa anapofika katika kituo cha afya au Hospitali asianze kuwaza ameenda kukaa sehemu hiyo kwa siku nzima na hivyo kusitisha shughuli zake nyingine, zingatieni mzunguko mzima wa utoaji huduma kwa wagonjwa kwa kuzingatia muda wa utaalam usiozidi masaa matatu". Amesema Waziri Mhagama.

Ameongeza kuwa muda huo ni kuanzia mgonjwa anapofika hospitalini kwa kuanza kujiandikisha, kumuona daktari, wakati anapatiwa matibabu na kupatiwa dawa kwamba mzunguko huo wa mgonjwa usizidi masaa matatu.

Ili kufanikisha hilo Waziri Mhagama amesisitiza uwepo wa matumizi ya TEHAMA pamoja mifumo kusomana ikiwa njia ndiyo njia pekee ya kuokoa muda na kutoa huduma bora kwa mgonjwa ikiwa ni sehemu ya kupunguza malalamiko ya mara kwa mara.

"Matumizi ya Tehama yatasaidia na kurahisisha mifumo ya matibabu na taarifa za mgonjwa kufanana na pia hata kurahisisha huduma kwa mgonjwa wakati atakapokuwa yupo hospitalini anatibiwa". Amesema Waziri Mhagama.

Kwa upande mwingine, Waziri Mhagama wamewataka watumishi wa afya kuwa na lugha ya staha wanapohudumia mgonjwa kwani lugha nzuri ni kichocheo kimojawapo cha kumpa ahueni mgonjwa na kujisikia vizuri.

Halikadhalika, amewahakikishia watumishi wa afya nchini kushirikiana nao ili kuweza kuhakikisha huduma bora za afya zinaendelea kutolewa kwa wananchi na mtumishi yeyote mwenye shida ya kumuona milango iko wazi.





# SERA YA CHAKULA NA LISHE KUKAMILISHWA ILI KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZA UDUMAVU

**Na Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Na WAF - DODOMA
Wizara ya afya inaendelea kukamilisha Sera ya chakula na lishe ili kukabiliana na changamoto ya utapiamlo na udumavu nchini kwa kujumuisha mapendekezo yaliyotolewa kwenye mkutano wa tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe nchini.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amesema hayo Agosti 31, 2024 wakati akimkaribisha Mgeni rasmi ambae ni Waziri wa Nchi ofisi ya Rais - TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa kwenye mkutano wa Nane wa Tathmini ya Mkataba wa Lishe na kutambulisha mpango wa Taifa wa uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto uliofanyika katika ukumbi wa Ofisi za Wizara ya Afya uliopo katika Mji wa Kiserikali (Mtumba) mkoani Dodoma.

"Tutaendelea kukamilisha Sera ya Taifa ya Chakula na Lishe ili iweze kutusaidia kutuongoza kukabiliana na changamoto mbalimbali za lishe na kwa kushirikiana na wadau kama Shirika la SANKU tumezindua kiwanda cha kuzalisha virutubishi nchini ili kurahisisha upatikanaji wa virutubishi nchini na unga utakaotumika na watoto wa mashuleni hapa nchini ni lazima uwe umeongezwa virutubishi." Amesema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama amesema katika kuhakikisha kwamba kuna muendelezo wa shughuli zilizokuwa zinafanywa na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Wizara imekamilisha maandalizi ya kuanzishwa kwa programu maalum ya lishe ambayo itachukua jukumu la TFNC.
Waziri Jenista pia amegusia suala la ubora wa mifumo ya kusajili mgonjwa pindi afikapo katika vituo vya kutolea huduma za afya na mfumo huo uwezeshe kuweka miadi na kupata huduma kwa wakati.

"Kazi kubwa ambayo ipo mbele yetu ni kuwa na mifumo imara ya kusimamia sekta ya afya ikiunganishwa na swala zima la lishe ili tuwe na matokeo chanya, tunatamani huduma za afya zinazotolewa kwenye Afya Msingi ziunganishwe moja kwa moja kwenye maeneo ya hospitali ya wilaya, Rufaa za mikoa, hospitali za kanda, hata hospitali kuu kwakua eneo hili la mifumo ni eneo kuu na sisi tunalipa kipaumbele, mifumo nayo izungumze ili tuweze kusomana na kuwasiliana". Amesema Waziri Mhagama

# HONGERENI KUPUNGUZA WAGONJWA KWENDA NJE YA NCHI




**Na Shabani Juma**
**DAR ES SALAAM**

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa amesema nchi wanachama wa Shirikisho la Watoa Huduma za Afya Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania zimejitahidi kuwekeza katika sekta ya afya na kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya Kanda kwa matibabu.

Ameyasema hayo Agosti 30, 2024 katika Mkutano wa 12 wa Shirikisho la Watoa Huduma za Afya Afrika Mashariki uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Njerere (JNICC). Dar es Salaam

Majaliwa ametoa wito kwa wawekezaji wa Sekta ya Afya kuwekeza nchini Tanzania kwa kuwa Serikali imetengeneza sera rafiki za uwekezaji hususan katika Sekta ya Afya kutokana na uhitaji wa huduma hizo nchini.

"Tunawakaribisha wawekezaji wote wenye nia ya kuwekeza kwenye sekta ya afya, Sera nzuri tunazo, Sheria na kanuni nzuri tunazo, mahitaji ya uwekezaji kwenye sekta ya afya ni makubwa na tunataka tupate teknolojia mpya na huduma za kibingwa."

Pamoja na hayo amewataka wadau wa afya wa kanda kujadili mbinu mbalimbali za kuimarisha mifumo ya afya na kuwa na mikakati ya pamoja ya kukabiliana na magonjwa.

"Tumieni jukwaa hili kuweka mikakati ya pamoja ya kupambana na magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ambukiza pamoja na magonjwa mapya yanayotokana na mabadiliko ya hali ya tabia nchi". Amesema Majaliwa.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel amesema kwa sasa ni wagonjwa wachache wanaosafiri nje ya nchi kwa ajili ya matibabu, kwani karibu magonjwa yote makubwa sasa yanaweza kutibiwa ndani ya Afrika Mashariki.

Amesema uwekezaji uliofanywa na serikali kuanzia ngazi ya chini umewezesha ugunduaji wa magonjwa yakiwa katika hatua za awali.

"Rufaa kwenda nje ya Nchi zimepungua kwa kiasi kikubwa kipindi cha nyuma watu waliokuwa wanafika Ocean road walikuwa kwenye hatua za mwisho za ugonjwa, lakini kutokana na uwekezaji sasa zaidi ya asilimia 70 ya wagonjwa wanakuja wakiwa na magonjwa katika hatua za awali" Amesema Dkt. Mollel

"Upo umuhimu wa kutengeneza Mfumo wa utoaji huduma katika Hospitali zetu za Rufaa ili mgonjwa akifika kupata huduma ya Tiba Jumuishi aweze kupata matibabu kwa wakati" amesema Dkt. Nyembea




# MSITUMIE NYARA ZA SERIKALI KWENYE TIBA ASILI

**Na Atley Kuni**
**MWANZA**

Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, ametoa wito kwa wataalamu wa tiba asili nchini kuachana na matumizi ya Nyara za Serikali kama ngozi za wanyama katika shughuli zao za kitabibu na badala yake wazingatie matumizi sahihi ya dawa zao.

Dkt. Mollel ametoa wito huo Agosti 31, 2024 wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Tiba Asili ya Mwafrila yalio fanyika Kitaifa jijini Mwanza na ratibiwa na Wizara ya afya chini ya baraza la tiba asili na tiba mbadala.

“Tunahitaji kuondokana na imani hizi potofu ili kunusuru maisha ya wanyama pamoja na binadamu. Hakuna sababu ya kuendeleza matumizi haya ya viungo vya wanyama kwa kuwa ni hatari kwa mazingira na ustawi wa binadamu, Sisi sote tunapaswa kukemea vitendo hivi, kulinda mazingira, na kuhakikisha tunafichua wenye vitendo viovu”. Amesema Dkt. Mollel

Aidha, Dkt. Mollel ameitaka Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kufanya tafiti za kina kwa wataalamu wa tiba asili ya Mwafrika kwani NIMR inapaswa kufanya tafiti za kina kuhusu vyanzo vya dawa zinazotumika na kuhakikisha kuwa zinatunzwa vizuri na kuendelezwa kuzalishwa kwa wingi kwenye huduma zao.

Kwa upande wake, Kaimu Mganga Mkuu, Dkt. Ahmad Makuwani, amekiri kuwa dawa zinazozalishwa na wataalamu wa tiba asili zimefanya maendeleo makubwa, huku mataifa mengine kama Angola yakizisajili kama dawa rasmi kwa matumizi ya binadamu.

Kilele cha maadhimisho haya kimewakutanisha waganga wa jadi na wataalamu wa tiba asili, huku kikiwa na lengo la kuboresha huduma za tiba asili na kutetea haki za wanyama katika utendaji wa tiba hizi.

# WIZARA YA AFYA NA DART WAJA NA MKAKATI WA ELIMU KUHUSU MPOX KWA ABIRIA

**DAR ES SALAAM**

Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wakala wa Mabasi yaendayo haraka (DART), Agosti 24, 2024 imetoa elimu juu ya ugonjwa wa Mpox kwa wananchi na abiria kituo cha mabasi hayo kilichopo Mbezi, Jijini Dar Es Salaam.

Akitoa Elimu hiyo Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma kutoka Wizara ya Afya, Dkt. Jonas Norman amesisitiza kwamba Wizara inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa elimu, hususani maeneo yanayokusanya watu wengi kama vyombo vya usafiri, na kuongeza kuwa ugonjwa huu haujafika nchini lakini ni muhimu elimu ikaendelea kutolewa ili tuwe tayari.

“Dalili za ugonjwa huo ni homa, kutokwa na vipele vyenye maji, uchovu wa mwili, maumivu ya mgongo kuvimba, mitoki ya mwili, maumivu ya misuli, na kuumwa kichwa. Pia ugonjwa huo unaweza kuambukizwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwingine ni kupitia kujamiiana na mtu aliye na ugonjwa huo, kushikana mikono, kupiga/kupigwa busu na mtu mwenye ugonjwa pamoja na kukumbatiana” amesema Dkt Norman

Kwa upande wake Mkurugenzi Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano kwa Umma wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka (DART), William Gatambii ameshukuru kwa kupewa mwongozo na Wizara ya Afya katika kutoa elimu ya afya kuhusu Mpox na wataendelea kutekeleza maelekezo yote ikiwemo kuhakikisha vyombo vya kunawia mikono vinarudishwa katika vituo vya abiria.

Wizara ya Afya inaendelea kutoa elimu kwa jamii ili kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu huku ikisisitiza wananchi kupiga simu bure kwenda namba 199 kwa msaada na elimu zaidi kuhusu ugonjwa wa Mpox.



# SERIKALI KUBORESHA UTARATIBU WA LIKIZO YA UZAZI KWA WANAWAKE




**Na Domina Jacob**
**DODOMA**

Serikali inaendelea na jitihada za kupunguza changamoto za unyonyeshaji kwa wanawake wenye mazingira magumu ya kunyonyesha watoto kutokana na matatizo ya kiafya kwa kufanya marekebisho ya utaratibu wa likizo ya uzazi kwa wanawake wanaojifungua watoto ambao hawajatimiza muda wa kuzaliwa au wenye matatizo makubwa ya kiafya.

Hayo yamesemwa Agosti 1, 2024 na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Tiba kutoka Wizara ya Afya, Dkt. Mwinyi Kondo wakati akimuwakilisha Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu, kwenye ufunguzi wa maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji duniani, yanayofanyika jijini Dodoma yanayoenda na kauli mbiu isemayo “Tatua Changamoto; Saidia Unyonyeshaji wa Watoto kwa Wote”.

Dkt. Mwinyi amesema maboresho hayo yatasaidia wanawake kupata muda wa kuwatunza vizuri watoto hao wenye matatizo na kupunguza hatari ya vifo kwa Watoto, pia yatasaidia kulinda ajira za wanawake ambao walikuwa wanapoteza ajira kutokana na kushindwa kurudi kazini baada ya likizo ya uzazi ya kawaida kumalizika.

“Natumia fursa hii kuwahimiza waajiri katika sekta za kiserikali, zisizo za kiserikali na jamii kwa ujumla kusaidia katika kutatua changamoto zinazowakabili wanawake iliwaweze kunyonyesha watoto na waajiri wahakikishe wanatenga sehemu maalum katika eneo la kazi kwaajili ya wafanyakazi wanawake wanaonyonyesha ili Watoto waweze kupata haki zao za kimsingi na kuwa na Afya na lishe bora”. Amesema Dkt. Mwinyi

Kwa upande wake Kamishna wa Kazi Msaidizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana na Watu wenye Ulemavu Bw. Andrew Ebron amesema Ofisi ya Waziri Mkuu ipo mstari wa mbele kuhakikisha sheria zote zinafuatwa kwa mwanamke na kuhakikisha anapata likizo ya siku 84 kwa mwanamke aliejifungua mtoto mmoja na siku 100 kwa mwanamke aliejifungua mtoto zaidi ya mmoja

Awali akimkaribisha Mgeni Rasmi, Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Lishe Bi. Neema Joshua ameeleza kuwa maadhimisho wiki ya unyonyeshaji maziwa ya mama kwa watoto yalianzishwa na kusimamiwa na Shirika la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 1992 duniani kote kwa lengo la kuhakikisha afya za watoto zinakuwa katika hali nzuri na lishe bora

“Tunakutana kila mwaka kwa ajili ya kukumbushana na kusisitizana lakini tunaangalia pia changamoto ambazo zipo na kuzitatua kwasababu changamoto bado zipo na zinahitaji kutatuliwa” Amesema Bi. Neema



# HAKIKISHENI MNATEKELEZA MAELEKEZO YA SERIKALI - DKT. JINGU

**Na Abdulwaheed Madenge**
**DAR ES SALAAM**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amewataka Wakuu wa Hospitali za Kanda, Maalumu na za Taifa pamoja baadhi ya Wakurugenzi wa Wizara ya Afya kutekeleza maelekezo ya serikali ya kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inayotumika katika taasisi inasomana na mifumo mingine ya Serikali.

Dkt. Jingu amesema hayo Agosti 2, 2024 akiwa kwenye kikao na Wakuu wa Hospitali za Kanda, Maalumu na za Taifa pamoja baadhi ya Wakurugenzi wa Wizara ya Afya kikao kilichofanyika katika Ofisi ndogo za Wizara ya Afya (NIMR) Jijini Dar es Salaam,

Amesema maelekezo hayo yanakuja kipindi ambapo serikali inazidi kusisitiza uboreshaji wa huduma za Afya na kuhakikisha huduma za Afya zinakuwa bora katika ngazi zote za Afya.

Katika kutekeleza maelekezo haya, ameelekeza kwamba utekelezaji uende sambamba na utumiaji wa mfumo wa tiba mtandao ambao Serikali imeshauweka katika Hospitali za ngazi ya mikoa ili kuboresha huduma.

Dkt Jingu ameongeza lengo ya jitihada zote za Serikali ni kupunguza adha za kupata huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kwa wananchi, ambapo uimara wa mifumo hiyo utachangia kupunguza rufaa za nje ya nchi kwa watanzania.

Kikao hicho pia kimehudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wizara ya Afya Issa Ng'imba, Mkurugenzi wa idara ya Tiba Dkt. Hamad Nyembea Mkurugenzi wa kitengo cha TEHAMA Wizara ya Afya Silvanus Ilomo Wizara ya Afya na baadhi ya wakurugenzi na Taasisi akiwemo Dkt. Peter Kisenge Mkurugenzi Taasisi ya Moyo ya Jakaya kikwete, Prof. Abel Makubi kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa na wengineo.




# 400 KUFANYIWA UPASUAJI WA MTOTO WA JICHO

**Na Aisha Swahibu**
**SONGWE**

Watu zaidi ya 400, wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho mkoani Songwe na maeneo jirani ikiwa ni jitihada za Serikali kusogeza huduma za kibingwa na Ubingwa Bobezi karibu na wananchi.

Huduma hiyo itakayotolewa Bure kwa muda wa Siku tano imeratibiwa na Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa Kushirikiana na Shirika la Hellen Keller.

Hayo yameelezwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Songwe Dkt. Ntufye Kapesa Agasti 5, 2024 wakati wa siku ya kwanza ya kambi ya huduma za matibabu ya upasuaji wa mtoto wa jicho katika Hospitali ya wilaya hiyo.

Wagonjwa wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho wametoka katika kata zote kumi na nane za Wilaya ya Songwe ambapo itadumu hadi Agosti 09,2024" amesema Dkt. Kapesa

Wagonjwa waliofuatwa kwenye kata zao kwa kutumia wahudumu wa afya ngazi ya jamii na usafiri bure, pia wanapokuwa hapa wao na ndugu zao watahudumiwa chakula bure na kurudishwa makwao, pia mpango huo utasaidia kuitangaza hospitali ya wiliya ya songwe kwani hospitali bado ni mpya" amesisiti Kapesa.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa wilaya ya Songwe, Godfrey Kawacha amesema jamii inafaidika na kufarijika kwa kupata huduma hiyo adimu kwa kuwa imewarahisishia kupata matibabu hayo kwa urahisi na bila gharama yoyote.

Bi. Pistina katumbi, Mkazi wa Kijiji cha mbagala mbuyuni, Wilaya yaSongwe, mkoa wa Songwe amesema amekuwa akisumbuliwa na hali ya kuto kuona kwa jicho lake moja kwa muda wa mwaka mmoja lakini kupitia kambi hiyo ameweza kufanyiwa matibabu bila gharama yoyote huku akimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwasogezea huduma hiyo karibu.

Awali Mganga mfawidhi mbali yakuelezea kambi itakavyokuwa ameishukuru serikali kwa kuendelea kutafuta wadau mbalimbali ili kuweza kutoa huduma za matibabu ya kibingwa kwa watanzania.

# TUMERIDHISHWA NA HUDUMA ZA AFYA KATIKA HOSPITALI YA RUFAA IRINGA

**Na Shaban Juma**
**IRINGA**

Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya Ukimwi inayoongozwa na Kaimu Mwenyekiti, Christine Mnzava, akiambatana na Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel na wajumbe wake, imefanya ziara katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa kwa ajili ya kuangalia hali ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Ziara hiyo imefanyika Agosti 06, 2024 katika mkoa wa Iringa ambapo Mhe. Mnzava amepongeza hospitali hiyo kwa jitihada kubwa za kuboresha huduma za afya na kutoa huduma bora wakati wote.

Aidha, ameeleza kuridhishwa kwake na maendeleo yaliyopatikana na juhudi zinazofanywa na watumishi wa hospitali katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya.

"Nawapongeza kwa juhudi zenu za dhati katika kuboresha huduma za afya. Huduma zenu zimeendelea kuwa bora na zenye viwango vinavyokidhi mahitaji ya wananchi wetu," amesema Mhe. Mnzava.

Aidha, amewataka watumishi wa hospitali hiyo kuendelea kuishi katika miiko ya kazi na kujitoa kwa ufanisi katika utendaji wao wa kazi. Ameeleza kuwa nidhamu na kujituma ni nguzo muhimu katika kufanikisha utoaji wa huduma bora za afya.

Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, ameongeza kuwa Serikali itaendelea kutoa msaada na rasilimali muhimu ili kuhakikisha huduma za afya zinaendelea kuboreka katika hospitali hiyo na maeneo mengine nchini.

Ziara hiyo imetoa fursa kwa wajumbe wa kamati kujionea hali halisi ya utoaji wa huduma za afya na kupokea taarifa za huduma za hospitali hiyo.



# HUDUMA NA ELIMU YA AFYA MAONESHO YA NANENANE DODOMA ZALETA FARAJA KWA WANANCHI

**Na. Domina Jacob**
**DODOMA**

Wananchi kutoka maeneo mbalimbali wanaotembelea banda la Wizara ya Afya katika Maonesho ya Wakulima na Wafugaji Kitaifa (Nanenane) Mkoani Dodoma, wamevutiwa na huduma zinazotolewa katika banda hilo.

Wakizungumza tarehe 7, Agosti, 2024 baada ya kutembelea banda la Wizara ya Afya kwenye maonesho ya nanenane Nzuguni Jijini Dodoma baadhi ya Wananchi hao akiwemo Jumanne Omary, Majaliwa Justine pamoja Bi. Yasinta Masaka wamesema huduma za Afya zinazotolewa katika banda la Wizara ya Afya zinavutia huku wakitoa wito kwa watu wengine kutumia fursa ya maonesho ya nanenane kupatahuduma za afya bila malipo.

"Huduma zao za afya ni nzuri sana hivyo nitoe wito kwa Wananchi wengine watumie fursa hii "amesema Jumanne Omary kutoka Homanyika Dodoma.

"Nimepima afya ya macho na kupewa ushauri mzuri na Watalaamu wa Afya tena kwa ukarimu mzuri mno niwasihi na wengine kuacha kulala nyumbani raha ya afya yako ni Banda la Wizara ya Afya"amesema Yasinta.

Ikumbukwe kuwa katika Banda la Wizara ya Afya huduma mbalimbali zinatolewa kuanzia Elimu ya Afya, Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa, Chanjo dhidi ya Homa ya ini, Uviko 19, pamoja na Chanjo dhidi ya Saratani ya Mlango wa Shingo ya Kizazi kwa wanawake Katika dawati la elimu na uhamasishaji kuna wataalam wa masuala ya Afya ya Akili, Lishe na Tiba Asili.

Kwenye dawati hili pia utapata elimu ya Ugonjwa wa Virusi vya UKIMWI pamoja na huduma za upimaji VVU, Elimu ya Ugonjwa wa Malaria pamoja na upimaji, Kifua Kikuu, na hapa tuna Maabara tembezi ambayo ina vifaa vya kisasa vya upimaji na wataalam wetu watakupima ewe mwananachi na kubaini endapo una maambukizi ya TB.

Huduma za uchunguzi wa awali wa Saratani ya Mlango wa Shingo ya Kizazi kwa wanawake, Saratani ya Matiti, Huduma za Uzazi wa Mpango njia zote zinapatikana.





# MAZINGIRA RAFIKI KWA WANAWAKE KUNYONYESHA MAENEO YA KAZI NI MUHIMU

**Na Cletus Sanga**
**DODOMA**

Waajiri katika sekta rasmi na zisizo rasmi wamehimizwa kuwawekea mazingira rafiki wanawake wenye watoto ili waweze kunyonyesha watoto wao katika maeneo yao ya kazi.

Hayo yamesemwa, Agosti 6, 2024, na Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Afya, Bi. Grace Sheshua, wakati akifungua mkutano wa maafisa rasilimali watu na sheria kutoka taasisi na mashirika ya serikali kuhusu masuala ya unyonyeshaji maziwa kwa wamama mahali pa kazi.

"Lishe ya mtoto katika siku 1000, yaani tangu kutungwa kwa mimba hadi mtoto anapofikisha umri wa miaka miwili, ndiyo msingi bora wa ukuaji wa mtoto kimwili na kiakili, amesema na kuongeza

"Madhara ya lishe duni, hasa udumavu, yanaathiri sana maendeleo ya rasilimali watu ya nchi hivyo ni muhimu kwa mtoto kunyonyeshwa maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo na kuendelea kunyonyeshwa huku akipatiwa chakula cha nyongeza hadi anapotimiza miaka miwili au zaidi," amesisitiza Bi. Grace.

Aidha, Bi. Grace amesema unyonyeshaji maziwa ya mama ni njia bora na salama ya kulisha watoto na mojawapo ya uwekezaji muhimu wa gharama nafuu unaoweza kufanyika kwa taifa lolote kwa mustakabali wa jamii bora kiuchumi na kijamii.

Kwa upande wake, Mratibu wa Kanda ya Kati wa TAWLA, Bi. Neema Mushi, amesema changamoto nyingine ni ukiukwaji wa haki za uzazi za wanawake wanaofanya kazi katika baadhi ya sekta rasmi na sekta zisizo rasmi. Hii inatokana na kukosekana kwa mazingira wezeshi katika mifumo ya kijamii ya kuwasidia wanawake waweze kuwanyonyesha watoto wao ipasavyo.

Naye Bi. Grace Moshi, Afisa Lishe kutoka Wizara ya Afya, ameeleza umuhimu wa lishe bora kwa mama mjamzito na anayenyonyesha, akisisitiza kuwa maandalizi mapema ni muhimu ili kuepuka changamoto kama ukosefu wa maziwa ya kutosha. Alizungumzia pia kuhusu faida za maziwa ya mama kwa afya ya mtoto, na umuhimu wa mtoto kunyonya maziwa hayo kwa miezi sita bila kuongezewa vyakula vingine.

# BMH YATAKIWA KUTEGUA KITENDAWILI ILI IWE HOSPITALI YA TAIFA

**Na Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu ameitaka Hospitali ya Kanda ya Kati ya Benjamini Mkapa kuendelea kuboresha zaidi hali ya utoaji na ubora wa huduma hususani zile za kibingwa na ubingwa bobezi ili iweze kupanda hadhi na kuwa Hospitali ya Taifa.

Dkt. Jingu ametoa kauli hiyo Agosti 9, 2024 wakati wa Ziara yake iliyolenga kutembelea Hospitali ya Benjamini Mkapa na kujionea utoaji wa huduma kwenye hospitali hiyo, ambapo akiwa hospitalini hapo amewasisitiza wataalamu hao kuona namna gani wanaboresha huduma ili kufikia hadhi ya Taifa.

“Hospitali ya Taifa kama mnavyofahamu kazi yake kubwa ni Kutoa huduma Bobezi na Ubora wa Huduma, sasa hapa tayari Mnahuduma za kutosha, Lazima tupambane usiku na mchana ili hospitali hii ipande hadhi na kuwa hospitali ya Taifa, amesema Dkt. Jingu na kuongeza

"BMH ni hospitali kubwa katika makao makuu ya nchi, katika hospital ya taifa ili iweze kutoa huduma zinazotakiwa kwa mazingira haya ya Makao Makuu ya Nchi, sasa lazima tuwe kituo ambacho kitaweza kukidhi mahitaji ya kitaifa zaidi na kutoa huduma hizo” amesisit8za Dkt. Jingu.

Dkt. Jingu Amesema njia pekee itakayo iwezesha Hospitali hiyo kupata hadhi ya Taifa ni wataalamu wa Hospitali kuziimarisha zaidi huduma mbalimbali inazotoa hususani zile za kibingwa na ubingwa bobezi.

“Lazima tuone namna gani tunaboresha zaidi huduma zetu katika Hospitali ya Benjamini Mkapa na naona tayari mmeshaonyesha jitihada, hapa kuna huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, tayari mna huduma kama 20 ukiacha zile nane ambazo ni Bobezi” amesema Dkt. Jingu.

“Kwa kuzingatia kuwa sisi ni watu wa familia moja, Kuna faida za Mashirikiano nazo ni nyingi ikiwemo wanafunzi wanaotoka Chuo kikuu cha Dodoma watapata sehemu sahihi za kujifunzia na bahati nzuri tatari mnawapa nafasi, na mwisho wa siku kama nchi tutanufaika maamuzi na tutapata watu ambao wameiva” Amesema Dkt. Jingu.

Akiwa hapo Dkt. Jingu pia ametembelea mradi wa ujenzi wa kituo cha Kansa Mradi wenye thamani ya Shilingi Bilioni 28 ambapo pia amemtaka Mhandisi wa mradi huo kuhakikisha unakamilika kwa wakati bila kuthiri ubora wa Mradi huo.






# WAANDISHI WA HABARI WAJENGEWA UWEZO JUU YA UNYONYESHAJI WA MAZIWA YA MAMA KWA MTOTO

**Na. Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa mtoto, lengo likiwa kuboresha afya ya watoto na akina mama.

Hayo yamesemwa Agosti 5, 2024 na Bi. Grace Moshi, Afisa Lishe kutoka Wizara ya Afya, wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa unyonyeshaji wa maziwa ya mama. Mafunzo haya yamefanyika jijini Dodoma na yanafuata kauli mbiu isemayo "Tatua Changamoto; Saidia Unyonyeshaji wa Watoto kwa Wote."

Bi. Grace ameeleza umuhimu wa lishe bora kwa mama mjamzito na anayenyonyesha, akisisitiza kuwa maandalizi mapema ni muhimu ili kuepuka changamoto kama ukosefu wa maziwa ya kutosha. Alizungumzia pia kuhusu faida za maziwa ya mama kwa afya ya mtoto, na umuhimu wa mtoto kunyonya maziwa hayo kwa miezi sita bila kuongezewa vyakula vingine.

Kwa upande wake, Bi. Elieth Deogratias, Afisa Lishe mwingine, ameongeza kuwa maziwa ya mama yanafaa zaidi kwa umeng'enywaji kwa mtoto mchanga kuliko maziwa ya wanyama. Amehimiza umuhimu wa mtoto kunyonya kwa kuhakikisha amekamata sehemu yote nyeusi ya nyonyo la mama, ili kuepuka maumivu kwa mama na gesi tumboni kwa mtoto.

Bw. Japhet Msoba, Afisa Lishe mwingine, amekanusha dhana potofu kwamba maziwa ya mama yanachacha, akisisitiza kuwa hakuna haja ya kuosha matiti mara kwa mara, kwani inaweza kusababisha michubuko kwa mama au mtoto anaponyonya.

Kwa upande wake, Bw. Paul Mabeja kutoka Nipashe ameishukuru Wizara ya Afya kwa ajili ya mafunzo haya, akisema kuwa yatawasaidia sana katika kufikisha ujumbe kwa wananchi kwa usahihi na kwa wakati muafaka. Ameongeza kuwa mafunzo haya yataimarisha uwezo wa vyombo vya habari katika kutoa taarifa sahihi kuhusu masuala ya afya, hivyo kuchangia kuboresha afya ya jamii kwa ujumla.




# AFYA WAMALIZA NANE NANE 2024 KWA KISHINDO, WAHUDUMIA WANANCHI ZAIDI YA 14,000

**Na Atley Kuni**
**DODOMA**

Wizara ya Afya imekuwa moja ya Wizara iliyofanya vizuri kwenye Maonesho ya Nanenane 2024 kwa kuhudumia wananchi zaidi 14,000 waliojitokeza katika Mabanda ya wizara hiyo na taasisi zake na kutwaa tuzo ya mshindi wa tatu wa Wizara Mtambuka zilizofanya vizuri wakati wote wa Maonesho.

Kwa mujibu wa takwimu zinaonesha mara baada yakukamilika kwa Maonesho hayo wingi wa wananchi walijitokeza walifika kupata chanjo ya Homa ya Ini wakiwepo 527 walipata chanjo aidha waliogundulika na Homa ya ini wapatao 53 walipewa rufani kwa ajili matibabu kabla yakupatiwa chanjo hiyo.

“Wananchi elfu 13077 wajitokeza, na wengine kupatiwa mipira ya kiume (Condom) zipatazo 2937 ziligawiwa kwa wananchi.

Kwa upande wa shinikizo la damu waliopima walikuwa elfu 5000 huku, 1663 walifanikiwa kupima Kifua Kikuu na waliogundulika na maambukizi walikuwa wawili ambao wote wameanzishiwa matibabu ya dawa.

Kwa upande wa waliojitokeza kupata elimu ya uzazi wa mpango walikuwa wananchi 260 na baadhi ya njia za uzazi walizo shauriwa ni ni pamoja na sindano, vidonge, vipandikizi, condom na kitanzi/lupu.

Huduma zilizotolewa katika muda wa siku zote kumi ni pamoja na Uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi, Elimu ya afya na ugawaji vipeperushi, uchunguzi wa Kifua kikuu (TB), Elimu ya uzazi wa mpango , upimaji wa maambukizi ya virusi vya UKIMWI, Elimu na uchunguzi juu ya afya ya Akili, upimaji wa shinikizo la damu pamoja na upimaji na ugawaji wa chanjo ya Homa ya Ini na Uviko 19 na pamoja na elimu juu ya Tiba asili na tiba lishe

Afisa Habari Mwandamizi kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Afya Atley Kuni, amesema kuwa Banda la Wizara ya Afya katika maonesho hayo zilikuwepo pia Taasisi zilizochini ya Wizara ambazo ni taasisi ya Muhimbili Orthopedic Institute, Hospitali ya Benjamin Mkapa Mamlaka ya vifaa Tiba na dawa TMDA, NHIF, Baraza la Uuguzi na Ukunga TNMC, pamoja na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali



# BILIONI 561 KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO UZALISHAJI BIDHAA ZA AFYA

**Na Hassan Kimweri**
**DODOMA**

Mwenyekiti wa kamati ya kudumu ya Afya na masuala ya UKIMWI Mhe. Elibariki Kingu ameishauri Wizara ya Afya kuendelea kuisimamia Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa kuipatia mtaji wa Bilioni 561.5 ili kukabiliana na changamoto za uzalishaji na uendelezaji wa viwanda vya dawa, vifaa na vifaa tiba ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hizo kwa wananchi.

Mhe. Kingu amesema hayo Agosti 20, 2024 kwenye kikao cha kamati ya kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI baada ya Wizara ya Afya kuwasilisha taarifa ya utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) pamoja na taarifa ya mikakati ya kukabiliana na changamoto ya Afya ya Akili nchini.

"Viwanda vya dawa, vifaa na vifaa tiba vinatakiwa kuendelezwa kwa kupatiwa mtaji wa kutosha ili kukabiliana na changamoto kama vile gharama kubwa za nishati pamoja na rasilimali watu." Amasema Mhe. Kingu

Kwa upande wake Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amesema Serikali kupitia Wizara ya Afya imepokea maelekezo ya kamati na Wizara imejipanga kupunguza gharama za uzalishaji katika viwanda vya dawa, vifaa na vifaa tiba ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa nyingi zenye ubora pamoja na kuboresha huduma za afya

"Gharama za uzalishaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba zimekua kubwa kutokana na ongezeko la Nishati za uzalishaji pamoja na rasilimali watu, hivyo kuwa na mbinu mbadala katika kupunguza gharama hizo ikiwa ni pamoja na kutumia gesi katika uzalishaji pamoja na vifaa saidizi." Amesema Waziri Mhagama

Katika hatua nyingine Waziri Mhagama amesema, Serikali imerudisha Diploma ya Uuguzi ya Afya ya Akili pamoja na 'Clinical Offices' ambayo itaongeza ufanishi kwa utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa Afya ya Akili maana changamoto hii imekua ikiongezeka kutokana na mtindo wa maisha.

Awali Wakati akiwasilisha taarifa ya mikakati ya kukabiliana na changamoto ya Afya ya Akili, Mkururenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza Dkt. Omari Ubuguyu amesema Serikali imewezesha ujenzi na ukarabati wa majengo ya kliniki za methadone Zaidi ya 16 zenye gharama zaidi ya Bilioni 5.

"Hospitali Taifa ya Afya ya Akili Mirembe imewezeshwa kupata Zaidi ya shilingi Bilioni 4 katika kipindi cha miaka 5 iliyopita ili kuweza kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika hospitali hiyo." Amesema Dkt. Ubuguyus

# TIBA ASILI KEMEENI VITENDO VYA UKATILI

**Na Atley Kuni**
**MWANZA**

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Saidi Mtanda amewataka watoa huduma za afya kwa njia ya tiba asili nchini kushirikiana na serikali kukemea na kutokomeza vitendo vya ukatili ndani ya jamii.

Mtanda ametoa kauli hiyo Agosti 28,2024 wakati akifungua Juma la Tiba asili na maadhimisho ya tiba asili kwa Mwafrika yanayofanyika kwenye viwanja vya Furahisha Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza.

"Ninyi Waganga wa Tiba asili mnamchango mkubwa katika kuimarisha afya za watanzania, hivyo tukiunganisha nguvu baina ya dawa zenu na zile za hospitalini wananchi watastawi kwakuwa na afya njema." Amesema Mhe. Mtanda na kuongeza

"Ni rai yangu, sisi wote tuungane kutokomeza vitendo vya ukatili wa mauwaji ya Albino na watoto ambayo yamekuwa yakiripotiwa hivi karibuni" amesisitiza Mtanda

Mkuu wa Mkoa Mtanda, ametumia fursa hiyo kuwataka waganga wa tiba asili wote kujisajili kwenye baraza la tiba asili na mbadala na kuhuisha leseni zao kila mwaka ili kuepuka kukumbwa na mkono sheria.

"Mimi ninaamini tiba hizi za asili zinapoboreshwa zinafanya kazi sawa na tiba hizi za kawaida na ndio maana Watanzania zaidi ya asilimia 60 nchini wanatumia tiba hizi na zinawasaidia, wote tunatambua kwamba tiba asili na tiba mbadala zimekuwa na mchango mkubwa kwa wananchi na ofisi ya mkuu wa mkoa kupitia idara ya afya "Amesema Mhe. mtanda

Kwa upande wake Mwenyekiti msaidizi baraza la tiba asili na mbadala nchini Dkt. Elizabeth Lema amesema waganga wa tiba hizo wametoka kwenye mfumo wa kufanya kazi zao kienyeji na sasa wanafanya kisasa na wakati mwengine wanatoa huduma jumuishi na wataalamu kutoka hospitali za kawaida ambao wanakiri kwamba tiba za asili zinamsaada mkubwa katika kutibu magonjwa mbalimbali.

Naye Msajiri wa baraza la tiba asili na mbadala Martin Mgogwa amebainisha kuwa baraza hilo pamoja na kuwasajiri linasimamia, kuthibiti na kuendeleza tiba asili nchini kwa kuhakikisha kila anayetoa huduma za tiba asili anasajiriwa pamoja na kuhuisha leseni kila mwaka katika eneo lake.



# TUENDELEE NA MIKAKATI YA KUZUIA MAGONJWA YA MLIPUKO KWA CHANJO



**Na Hassan Kimweri**
**Brazzaville, Congo**

Rais wa Congo Brazzaville, Mhe. Denis Sassou Ng'uesso amesisitiza umuhimu wa kuendelea na mikakati ya kuzuia magonjwa ya milipuko kwa kutumia chanjo kwa kuwa magonjwa hayo hutokea wakati wowote.

Rais Ng'uesso amesema hayo Agosti 26, 2024 wakati akifungua Mkutano wa Afya wa 74 wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika uliowakutanisha Mawaziri kutoka katika nchi hizo.

"Nchi wanachama bado inakabiliana na magonjwa, majanga na matukio mbalimbali ambayo yanahitaji nguvu ya pamoja, tuendelee kuweka mikakati ya Afya ya Msingi ili kukabiliana na majanga haya." Amesema Rais Ng'uesso

Amesema, magonjwa hayo mengi ya mlipuko yanatokana na Mabadiliko ya Tabia Nchi ambayo yanahitaji nguvu ya pamoja kwa usalama wa mazingira yetu na usalama wa binadamu kwa ujumla.

Kwa upande wake Waziri wa Afya Tanzania Mhe. Jenista Mhagama wakati akichangia mada katika mkutano huo amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inathamini usaidizi wa WHO katika kupambana na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Amesema, pamoja na maandalizi ya dharura, Serikali ya Tanzania inatoa shukrani za dhati kwa 'Regional Director' na WHO ambapo kwa pamoja inawezekana kujenga Afrika yenye ustahimilivu zaidi.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunampongeza Mkurugenzi kwa uongozi na kuipongeza kwa kuongoza vizuri Afrika katika 'International Health Regulations' (IHR) na tunatazamia kukamilishwa kwa mkataba wa janga hili." Amesema Waziri Mhagama

Nae, Waziri wa Afya Congo Brazzaville, Mhe. Gilbert Mokoki amesisitiza nchi wanachama kuweka kipaumbele cha fedha za kusaidia Shirika la Afya Duniani kupitia Programu ya 14 ya Shirika hilo.

"Tuweke mikakati ya pamoja ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwemo ugonjwa wa MPOX ili kuwa na Afya kwa wote." Amesema Waziri Mokoki

# DKT. MOLLEL AWAPONGEZA NTLP, NASHCOP KWA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO KWA WELEDI

**Na Majid abdulkarim**
**DODOMA**

Naibu Waziri wa Afya Mhe. Godwin Mollel tarehe 27 Agosti, 2024 amekutana na watumishi wa Programu kutoka Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) pamoja na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCoP) katika ofisi za Wizara ya Afya zilizopo kilimani jijini Dodoma.

Akiwa katika kikao kazi hicho ambacho Dkt. Mollel aliambatana na Naibu Katibu Mkuu Bw. Ismail Rumatila na Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali Dkt, Ahmed Makuwani amewapongeza watumishi wa Programu hizo chini ya Mkuu wa Programu Dkt. Catherine Joachim kwa kutekeleza vizuri shughuli za kupambana na magonjwa hayo nchini.

Pia Dkt.Mollel, amewataka watumishi wa Programu kuendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa weledi mkubwa ili kuleta tija na ufanisi katika kufikia malengo ya nchi ya kutokomeza magonjwa hayo.

Kikao hicho kiliitishwa kwa lengo la kupokea taarifa za utekelezaji na kujadili mambo mbalimbali yanayohusu udhibiti wa magonjwa hayo nchini.

Aidha, Naibu Katibu Mkuu Bw. Rumatila amewapongeza watumishi wa Programu hizo kwa kuwa na jitihada za kupambana na magonjwa hayo pamoja na kuwataka watumishi hao kuongeza kasi katika kuwatafuta wagonjwa wanaokosekana na kuwaweka kwenye matibabu ili kuzuia kuenea kwa magonjwa haya katika jamii.

Kwa upande wake Dkt. Catherine Joachimu amewashukuru viongozi hao kwa kutenga muda na kukutana na watumishi wa Programu hizo hatua ambayo itaongeza hamasa na chachu kwa watumishi katika kutekeleza mikakati ya nchi ya Kutokomeza magonjwa hayo ifikapo mwaka 2030.






# TANZANIA YAUNGA MKONO MKAKATI WA KIKANDA WA USALAMA WA AFYA NA DHARURA (2022-2030)

**Na Hassan Kimweri**
**Brazzaville, Congo**

Tanzania inaunga mkono mkakati wa kikanda wa usalama wa afya na dharura kwa kipindi cha 2022–2030 kupitia hatua za utekelezaji wa miradi muhimu, kuanzisha mpango wa wafanyakazi wa afya ya jamii ulio jumuishi na kuratibiwa, na kupanga kwa ajili ya kurejesha na kuimarisha mifumo ya afya iliyoathiriwa na janga la COVID-19.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amesema hayo Agosti 28, 2024 wakati akitoa taarifa ya Tanzania kwenye ajenda ya kipengeke cha 12 kwenye kikao cha 74 cha Shirika la Afya Duniani (WHO-AFRO) ambacho kinajadii mbinu bunifu za kuimarisha muundo wa Kimataifa wa maandalizi na mwitikio wa dharura za kiafya katika Kanda ya Afrika ya WHO.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaunga mkono na inatambua taarifa zilizotolewa na inapongeza Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa mafanikio yake bunifu katika kuimarisha maandalizi na mwitikio wa dharura za kiafya katika Kanda ya Afrika ambapo inakadiriwa kuwa na matukio 102 kila mwaka." Amesema Waziri Mhagama
Waziri Mhagama amesema, kwa kuendana na mkakati huo, Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuboresha uwezo wa kugundua, kujiandaa, na kuitikia dharura za kiafya (EPR) ambapo amependekeza zichukuliwe jitihada za kuanzisha, kuhamasisha, na kutetea matumizi ya vituo vya umahiri na vituo vya maandalizi na mwitikio wa dharura katika Kanda ndogo wakati wa dharura za kiafya.

"Hili limeonyeshwa na ufanisi wetu katika kushughulikia mlipuko wa 'Marburg Virus Disease' mwaka 2023 na matokeo chanya ya tathmini ya pamoja ya nje ya pili (JEE) iliyofanyika mwezi Agosti 2023." Amesema Waziri Mhagama

Aidha, Waziri Mhagama amesema, kutokana na ongezeko la mara kwa mara na ugumu wa dharura, Tanzania inahimiza WHO kuendelea kutoa msaada wa kimkakati na kiutendaji ili kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika tathmini za hatari za mipakani, ufuatiliaji, ujasusi wa magonjwa, pamoja na usambazaji wa taarifa kwa wakati.

"Pia tunaiomba WHO kuhamasisha usaidizi wa washirika na kuhimiza ufadhili wa ndani ili kukabiliana na changamoto za rasilimali kwa miradi muhimu na operesheni za mwitikio." Amesema Waziri Mhagama

# HONGERA

**Dkt. Faustine Ndugulile**
**Kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika**



*Building a Healthier Africa, Together.*

wizara_afyatz www.moh.go.tz




**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI AGOSTI, 2024**

@wizara_afyatz www.moh.go.tz